

---

SURA YA 290

---

SHERIA NDOGO

---

Zimetungwa chini ya vifungu vya 7(k) na 16(1)

SHERIA NDOGO ZA ADA NA USHURU ZA HALMASHAURI YA WILAYA  
YA MUHEZA ZA MWAKA, 2014  
**SEHEMU YA KWANZA**  
**MASHARTI YA AWALI**

- Jina
1. Sheria Ndogo hizi ziiitwe Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Muheza za Mwaka 2014 na zitaanza kutumika mara baada ya Kutangazwa katika Gazeti la Serikali.
- Matumizi
2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza.
- Tafsiri
3. Katika Sheria Ndogo hizi ispokuwa kama itaelezwa vinginevyo, tafsiri za maneno zitatumika kama ifuatavyo:-
- Sura ya 290
- “Sheria” maana yake ni Sheria za Fedha za Serikali za Mitaa;
- “Afisa Muidhiniwa” maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeidhiniwa kutekeleza chochote chini ya Sheria Ndogo hizi;
- “Ada” maana yake ni ada inayotozwa chini ya sheria ndogo hizi kwaajili ya vibali au leseni mbalimbail;
- “ushuru” maana yake ni ushuru unaotozwa chini ya sheria ndogo hizi kwaajili ya huduma zinazotolewa na halmashauri;
- “Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Muheza;
- “Mkurugenzi maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri na itajumuisha Kaimu Mkurugenzi;
- “Mwenyekiti” maana yake ni Mwenyekiti wa Halmashauri;
- “Mlipa ada/ushuru” maana yake ni yeyote anayehusika na

upataji wa vibali, leseni, au huduma za Halmashauri;

“Mawasilisho” maana yake ni mawasilisho yote ya kodi, nyaraka au maelezo yoyote yanayohitajika kuwasilishwa Halmashauri ambayo yanayofanywa na mlipa kodi;

“Waziri” maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa;

“Mwaka wa fedha” maana yake ni Mwaka wa Fedha kama unavyotambuliwa Serikali;

## **SEHEMU YA II JINSI YA KUTOZA/ KUKUSANYA KODI**

Ada/usuru

- 4 (1) Halmashauri itatoza ada na usuru mbalimbali kwaajili ya bidhaa au shughuli za kiuchumi au huduma zinazotolewa kwa malipo katika eneo lake zitakazojumuisha utoaji wa leseni au vibali mbalimbali kama inavyooneshwa katika jedwali la sheria ndogo hzi.
- (2) Ada au usuru utakaotzwa chini ya sheria ndogo hizi utalipwa kabla ya kupata huduma husika au vinginevyo kama itakavyoelekezwa na mkurugenzi kwa maandishi;
- (3) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kubadilisha viwango kwa asilimia ishirini na tano [25%] kadri itakavoonekana katika kila kipindi cha miaka mitatu na kwa masharti kwamba kusudio la mabadiliko hayo litatolewa kwa wadau angalau siku ishirini na moja kabla ya kuanza kutumika.

Muda na utaratibu wa kulipa ada/usuru

- 5 (1) Malipo yote ya ada au usuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi kutegemeana na uwezo wa mdau husika na maelekezo yatakayotolewa na mara kwa mara na Mkurugenzi;
- (2) Malipo ya ada au usuru unaotzwa kwa mujibu wa sheria ndogo hizi vitalipwa kwa Halmashauri au wakala wake ambaye atatoa stakabadhi ya malipo kama kielelezo cha malipo;
- (3) Ni wajibu wa mdau yeyote mlipa ada au usuru kudai na kuhakikisha anapewa stakabadhi halali kwa malipo anayotoa;

8. (1) Halmashauri inaweza kutangaza zabuni ya ukusanyaji wa ada au ushuru na kumteua wakala ikiwa ni mtu binafsi, kampuni au taasisi ambaye ataingia mkataba wa uwakala na Halmashauri kwaajili ya kukusanya ada au ushuru husika.
- (2) Kwa madhumuni ya kurahisisha ukusanyaji na kuepuka gharama za ukusanyaji wa ada au ushuru, pale ambapo Halmashauri itaona inafaa kufanya ubinafsishaji wa ukusanyaji wa ada au ushuru, itawajibika kufanya uchambuzi wa kina utakaobainisha wazi kiasi cha ada au ushuru unayoweza kupatikana kuhusiana na chanzo hicho na kamwe Halmashauri haitaruhusiwa kuingia mkataba na wakala kabla haijafanya uchambuzi wa kina kuhusiana na uwezo wa upatikanaji fedha wa chanzo hicho.
- (3) Wakala atakayeteuliwa na Halmashauri kutekeleza jukumu lolote chini ya Sheria Ndogo hizi, atawajibika kusimamia ukusanyaji huo kwa viwango vilivyoainishwa na Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hizi na kamwe hataruhusiwa kutoza viwango tofauti na vilivyobainishwa chini ya Sheria Ndogo hii.
- (4) Mtu yeyote atakayeteuliwa kama wakala chini ya Sheria Ndogo hii, atakuwa na majukumu ya kukusanya ada au ushuru na kumshitaki mtu yeyote atakayeshindwa kwa makusudi kulipa ada au ushuru unaotakiwa kulipwa kwa wakala huyo kwa muda unaotakiwa katika Mahakama yenye Mamlaka ya kusikiliza shauri hilo kama madai.
- (5) Wakala atakuwa na majukumu kwa Halmashauri yafuatayo:-
  - (a) Kukusanya na kupokea ada au ushuru kwa kiwango kilichoainishwa katika Sheria Ndogo hizi kwa niaba ya Halmashauri katika eneo ambalo ameteuliwa kukusanya ada au ushuru husika;
  - (b) Kuwasilisha makusanyo yote aliyowajibika kukusanya kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala;
  - (c) Kumchukulia hatua za kisheria mtu yeyote ambaye atakiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi;

9. Mkurugenzi anaweza kumuita mlipa ada au ushuru yeyote afike mbele yake au mbele ya Afisa muidhiniwa kwa muda unaofaa na kutoa maelezo yanayohitajika kuhusiana na malipo ya ada au ushuru.

Uwezo wa Mkurugenzi  
kufifilisha kosa

10. Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa kwa kumtoza mlipa ada au ushuru aliyetenda kosa, chini ya Sheria Ndogo hizi ikiwa mlipa ada au ushuru huyo amekiri kwa maandishi kwa Mkurugenzi, kuwa ametenda kosa hilo na kuwa atalipa ada au ushuru anaodaiwa pamoja na faini na kisha atapatiwa stakabadhi ya malipo hayo.

Kufungua Shauri  
Mahakamani

11. Bila ya kuathiri Sheria Ndogo ya 10 na Sheria Ndogo ya 12, endapo mlipa ada au ushuru yeyote atashindwa kulipa ada, ushuru au na adhabu, Halmashauri itafungua shauri la madai kwa njia ya mkato [summary procedure] katika Mahakama yenye uwezo wa kusikiliza shauri hilo.

Hati ya  
Kukamata  
Mali

12 (1) Bila ya kuathiri Sheria ndogo ya 10, 11 na 12, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kisheria kuomba katika Mahakama yenye Mamlaka katika eneo la Halmashauri, kwa kutumia hati iliyopo katika jedwali la kwana la Sheria Ndogo hizi, hati ambayo itaonyesha jina la mlipa ada au ushuru na anuani ya mlipa ada au ushuru na kumtaka mhusika huyo kulipa deni na faida anayodaiwa kulingana na Sheria Ndogo hizi.

(2) Hati atakayopewa mlipa ada au ushuru na mahakama itakuwa na mamlaka ya mamlaka kisheria ya kukamata na kuuza mali inayoondosheka ya Mlipa ada au ushuru na kila hati ya madai ambayo itapelekwa Mahakamani kwa nia ambayo imeelezwa katika Sheria Ndogo hizi, itakuwa ni uthibitisho kamili wa maelezo ya madai yaliyoelezwa chini ya hati hiyo.

**SEHEMU YA III**  
**MAKOSA, ADHABU NA JINSI YA KUCHUKUA**  
**HATUA ZA KISHERIA**

Deni

13. (1) Ada au ushuru au na faini yoyote ambayo Halmashauri inadai kwa mtu yoyote, kikundi cha watu, Kampuni au Taasisi chini ya Sheria ndogo hizi itakuwa ni deni la Halmashauri na litalipwa kutoka kwa mtu yeyote, kikundi cha watu, kampuni au Taasisi kupitia kwa Mkurugenzi au Afisa yeyote aliyeidhiniwa chini ya Sheria Ndogo hizi kwa niaba ya Mkurugenzi.

(2) Bila ya kuathiri maelezo ya jumla ya Sheria Ndogo ya 13(1) hapo juu, kuhusiana na jinsi ya kudai deni lolote la Halmashauri, ikiwa Afisa yeyote aliyeidhiniwa na Mkurugenzi atafungua shauri katika Mahakama yenye Mamlaka ya kusikiliza shauri na ataandaa hati ya malalamiko ambayo itaeleza uzito wa kosa na maombi.

- (3) Kutokana na hati ya madai ya deni la Halmashauri pamoja na faida 20% ya deni hilo iliyoandaliwa dhidi ya mdaiwa yeyote kupelekwa Mahakamani.
- (4) Kila hati ya madai ambayo itapelekwa Mahakamani kwa njia ambayo imeelezwa katika Sheria Ndogo hii, itakuwa ni uthibitisho kamili wa madai yaliyoelezwa katika hati hiyo.
- Mdaiwa anaposhindwa kulipa deni 14. Ikiwa mdaiwa yeyote atatozwa faini chini ya Sheria Ndogo ya 13 hapo juu na akashindwa kulipa deni hilo kwa wakati, Mahakama itaendelea kusikiliza shauri hilo kama kawaida inavyosikiliza mashauri mengine na itatumia mamlaka yake eidha iongeze adhabu au itoe adhabu ya kifungo kwa mdaiwa yeyote kwa muda usiopungua miezi sita au vyote kwa pamoja faini na kifungo.
- Kukusanya ada Au ushuru bila Ruhusa 15. Mtu yeyote ambaye-
- (a) Hajaruhusiwa na Halmashauri kwa maadishi kukusanya ada au ushuru unayokusanywa chini ya Sheria Ndogo hizi;
- (b) amekusanya au amejaribu kukusanya ada au ushuru kwa kiwango ambacho hakijatajwa chini ya Sheria Ndogo hizi;
- Atakuwa ametenda kosa chini ya sheria Ndogo hizi na akipatikana na hatia ya kufanya kosa hilo, atalipa faini ya shilingi laki tatu au kifungo cha miezi sita au vyote viwili kwa pamoja faini na adhabu ya kifungo hicho.
- Hatua za kisheria 17. Mashauri yote kuhusiana na malipo ya ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi au kuhusiana na adhabu yoyote chini ya Sheria Ndogo hizi, yanaweza bila kuathiri haki ya mtu yeyote au mamlaka nyingine ya kufungua shauri la jinai, litafunguliwa na Halmashauri kuhusiana na makusanyo ya ada au ushuru mbele ya Mahakama yoyote yenye Mamlaka ya kusikiliza shauri hilo.
- Sheria Na. 49/ 1966 19. Bila ya kuathiri maelezo ya jumla ya Sheria Ndogo hizi, katika kudai deni la ada au ushuru, Halmashauri itatumia Sheria ya Kanuni za Mwenendo wa Madai [Civil Procedure Code Act] na Halmashauri pia itapata faida kutokana na kiasi kinachotolewa na Benki kwa wakati husika.
- Makosa 20. Mtu yeyote ikiwa ni mlipa ada, mlipa ushuru, wakala au mkusanya ada au ushuru ambaye:-
- (a) ameshindwa, amedharau, au amekaidi kulipa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi;
- (b) ameshindwa, amedharau, au amekaidi kuwasilisha kodi aliyokusanya kwa Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hizi;

- (c) Ameshindwa kuleta taarifa zozote ambazo zinahitajika kuthibitisha makusanyo yake au ada au ushuru unaohitajika kwa Halmashauri;
- (d) Atamshawishi mtu yeyote asilipe au atamzuia mkusanya ada au ushuru yeyote kufanya kazi yake;
- (e) Ameshindwa kuwasilisha ritani, taarifa, kabrasha, au maelezo yoyote yanayohitajika chini ya Sheria Ndogo hizi;
- (f) Ameshindwa kuweka vizuri kumbukumbu, vitabu, hesabu au maelezo yoyote yanayohitajika chini ya Sheria ndogo hizi;
- (g) Ametengeneza, ametayarisha au ameidhinisha utengenezaji, utunzaji na utunzaji wa hesabu au nyaraka za uongo;
- (h) Amemzuia Mkurugenzi au Afisa Muidhiniwa kutekeleza kazi yake chini ya Sheria Ndogo hizi.
- (i) Amefanya biashara eneo lisilo rasmi au eneo ambalo halijatengwa kwa matumizi husika na kupelekea Halmashauri kukosa mapato chini ya Sheria Ndogo hizi.

Atakuwa ametenda kosa na akifahamika kutenda kosa hilo atahukumiwa kulipa faini ya shilingi laki tatu au kifungo cha mwaka mmoja au vyote viwili faini na kifungo.

---

Jedwali la kwanza la sheria ndogo

---

Ada ya machinjio na ukaguzi wa nyama mnadani/machinjioni

---

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 4*

| Na. | SAFU YA KWANZA: aina ya mfugo | SAFU YA PILI: kiasi cha ada |
|-----|-------------------------------|-----------------------------|
| 1.  | Ng'ombe                       | 2,500/= kwa ng'ombe mmoja   |
| 2.  | Mbuzi                         | 1,500/= kwa mbuzi mmoja     |
| 3.  | Kondoo                        | 1,500/= kwa kondoo mmoja    |
| 4.  | Nguruwe                       | 3,500/= kwa nguruwe mmoja   |

Jedwali la pili la sheria ndogo

Ushuru wa mifugo mnadani

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 4*

| <b>Na.</b> | <b>SAFU YA KWANZA: aina ya mfugo</b> | <b>SAFU YA PLI: kiasi cha ushuru</b> |
|------------|--------------------------------------|--------------------------------------|
| 1.         | Ng'ombe                              | 2,000/= kwa ng'ombe mmoja            |
| 2.         | Mbuzi                                | 1,000/= kwa mbuzi mmoja              |
| 3.         | Kondoo                               | 1,000/= kwa kondoo mmoja             |
| 4.         | Nguruwe                              | 3,000/= kwa nguruwe mmoja            |

Jedwali la tatu la sheria ndogo

Ada kwa watoa huduma za tiba asilia na wauzaji dawa za jadi

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 4*

| <b>Na.</b> | <b>SAFU YA KWANZA</b>       | <b>SAFU YA PLI: kiasi cha ushuru</b> |
|------------|-----------------------------|--------------------------------------|
| 1.         | Waganga wa jadi             | 30,000/= kwa mwaka/ 2,500 kwa mwezi  |
| 2.         | Taasisi                     | 30,000/= kwa mwaka                   |
| 3.         | Wauzaji wa dawa za kienyeji | 300/= kwa siku 9,000 kwa mwezi       |

Jedwali la nne la sheria ndogo

Ushuru wa stendi, kuegesha magari yanayoingia sokoni, mnadani na gulioni

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 4*

| <b>Na.</b> | <b>SAFU YA KWANZA</b>                                | <b>SAFU YA PLI: kiasi cha ushuru</b> |
|------------|--|--------------------------------------|
| 1.         | Basi abiria 40-60                                    | 2,000 kwa siku                       |
| 2.         | Basi la abiria 20-40                                 | 1,500/= kwa siku                     |
| 3.         | Hiece  | 500/= kwa siku                       |
| 4.         | Tax  | 500/= kwa siku                       |
| 5.         | Magari binafsi yasiyo ya biashara                    | 200/= kwa siku                       |
| 6.         | Gari dogo la mizigo [pick up/ lorry chini ya tani 7] | 2,000/= kwa siku                     |
| 7.         | Gari kubwa zaidi ya tani 7                           | 2,500/= kwa siku                     |

Jedwali la tano la sheria ndogo

Ushuru wa mazao ya misitu

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 4*

| Na. | SAFU YA KWANZA                             | SAFU YA PLI: kiasi cha ushuru      |
|-----|--|------------------------------------|
| 1.  | Mkaa                                       | 1,000 kwa gunia                    |
| 2.  | Mbao                                       |                                    |
|     | Urefu chini ya ft 10 [ft 0-9]              | 300/= kwa kwa kila mbao            |
|     | Urefu zaidi ya futi 9 [ft 10 na kuendelea] | 500/= kwa kwa kila mbao            |
| 3.  | Kuni                                       | 500/= kwa ujazo wa mita 1 ya ujazo |
| 4.  | Nguzo                                      | 100/= kwa nguzo moja               |
| 5.  | Fito                                       | 100/= kwa ujazo wa mita 1 ya ujazo |
| 6.  | Asali                                      | 100/= kwa lita                     |
| 7.  | Nta  | 500/= kwa kilo                     |
| 8.  | Kibali cha kukata/kuvuna mti               | 1,000/= kwa mti mmoja              |

Jedwali la sita la sheria ndogo

Ushuru wa bodaboda

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 4*

| Na. | SAFU YA KWANZA                                | SAFU YA PLI: kiasi cha ushuru |
|-----|---|-------------------------------|
| 1.  | Ushuru wa bodaboda kwa mzunguko wa siku nzima | 300 kwa siku                  |

Jedwali la saba la sheria ndogo

Ada ya mbao za matangazo

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 4*

| Na. | SAFU YA KWANZA  | SAFU YA PLI: kiasi cha ushuru |
|-----|---|-------------------------------|
| 1.  | Sm 1 ya eneo la mraba la kila bango la viwanda/mashirika binafsi        | 20/=                          |
| 2.  | Biashara za kati (vituo vya mafuta, nyumba za wageni, hotel)            | 10,000 -30,000/=              |
| 3.  | Biashara ndogondogo zenye mabango na zisizo na mabango                  | 5,000/=                       |
| 4.  | Yanayong'aa usiku ukiondoa ya sehemu (1)                                | 50,000/= -100,000/=           |
| 5.  | Aina ya matangazo ya maandishi yatatozwa katika maeneo yote ya biashara | 2,000/=                       |
| 6.  | Matangazo yabiashara kwa kutumia vipaza sauti / muziki                  | 15,000/= kwa siku             |

Jedwali la nane la sheria ndogo

Ada ya kukodisha ukumbi wa Halmashauri

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 4*

| Na. | SAFU YA KWANZA  | SAFU YA PLI: kiasi cha ushuru |
|-----|---|-------------------------------|
| 1.  | Ukodishaji ukumbi kwaajili ya semina za mashirika na miradi | 70,000/= kwa siku             |
| 2.  | Matumizi ya ukumbi kwaajili ya asasi za kiraia              | 50,000/= kwa siku             |
| 3.  | Matumizi binafsi  | 70,000/= kwa siku             |
| 4.  | Kukodisha viti  | 200/= kwa kiti                |



Jedwali la tisa la sheria ndogo

Ada ya magobole

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 4*

| <b>Na.</b> | <b>SAFU YA KWANZA</b> | <b>SAFU YA PLI: kiasi cha ushuru</b> |
|------------|-----------------------|--------------------------------------|
| 1.         | Gobole                | 5,000/= kwa mwaka                    |

Jedwali la kumi la sheria ndogo

Ada ya kukodisha magari na mitambo ya halmashauri/ushuru wa bima

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 4*

| <b>Na.</b> | <b>Ukodishaji Magari/Mitambo</b>                     |                   |
|------------|--|-------------------|
| 1.         | Viwango vitakavyotamkwa na halmashauri mara kwa mara |                   |
| 2.         | Ushuru wa bima                                       | 2.5% ya makusanyo |

Jedwali la kumi na moja la sheria ndogo

Ada ya ukaguzi wa afya

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 4*

| <b>Na.</b> | <b>SAFU YA KWANZA</b>                                  | <b>SAFU YA PLI: kiasi cha ushuru</b> |
|------------|--|--------------------------------------|
| 1.         | Nyumba za starehe, baa na vilabu vya pombe za kienyeji | 5,000/= kila baada ya miezi 6        |
| 2.         | Nyumba za kulala wageni                                | 5,000/= kila baada ya miezi 6        |
| 3.         | Maduka ya bidhaa                                       | 2,000/= kila baada ya miezi 6        |
| 4.         | Nyumba za kutengeneza na kuuzia vyakula na nyama choma | 3,000/= kila baada ya miezi 6        |
| 5.         | Ukaguzi wa maombi ya kufungua biashara                 | 5,000/=                              |
| 6.         | Ukaguzi wa viwanda vikubwa                             | 100,000/=                            |
| 7.         | Ukaguzi wa viwanda vya kati na karakana                | 50,000/=                             |
| 8.         | Ukaguzi wa viwanda vidogo                              | 20,000/=                             |
| 9.         | Masuala ambayo hayajatajwa na yanahitaji ukaguzi       | 3,000/=                              |

Jedwali la kumi na mbili la sheria ndogo

Ada ya nyumba za wageni

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 4*

| Na. | SAFU YA KWANZA                                    | SAFU YA PLI: kiasi cha ada |
|-----|---|----------------------------|
| 1.  | Wageni walioingia katika nyumba ya wageni         | 5% ya malipo kwa chumba    |
| 2.  | Faini kwa mmiliki mwenye vitabu 2/ kwaudanganyifu | 300,000/=                  |

Jedwali la kumi na tatu la sheria ndogo

Ada ya usajili wa tax na bodaboda na daladala zinazozunguka muheza mjini

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 4*

| Na. | SAFU YA KWANZA      | SAFU YA PLI: kiasi cha ushuru |
|-----|---------------------|-------------------------------|
| 1.  | Usajili wa tax      | 20,000/=                      |
| 2.  | Usajili wa daladala | 20,000/=                      |
| 3.  | Usajili wa bodaboda | 5,000/=                       |

Jedwali la kumi na nne la sheria ndogo

Ada ya kibali cha shughuli za utamaduni

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 4*

| Na. | SAFU YA KWANZA   | SAFU YA PLI: kiasi cha ada  |
|-----|--|---|
| 1.  | Disko siku za sikukuu na au siku yoyote ya juma                    | 5,000/= kwa siku  |
| 2.  | Tiba za jadi   | 10,000/= kwa mwaka  |
| 3.  | Michezo na sanaa za maonyesho, ngoma, sarakasi, michezo ya kuigiza | 2,000/= kwa siku  |
| 4.  | Shughuli za sanaa za ufundi/ uchoraji picha za rangi na vinyago    | 1,000/= kwa onyesho   |
| 5.  | Vikundi vya sanaa za maonyesho na sanaa za ufundi                  | 10,000/= kwa mwaka  |
| 6.  | Kucheza meza za pool   | 10,000/= kwa mwaka  |
| 7.  | Kuendesha promotion katika bar au hotel                            | 15,000/= kwa siku   |
| 8.  | Sehemu za makumbusho au za kihistoria kwa mtu mmoja                | (a) 1,000/= mtu mzima raia<br>(b) Mtu mzima asiye raia 10 usd<br>(c) Mwanafunzi wan je ya nchi 5usd<br>(d) Mwanafunzi wa ndani ya nchi - bure |
| 9.  | Kuendesha utafiti wa masuala ya kale                               | (a) Raia – 50,000/=<br>(b) Asiye raia – usd 70  |

Jedwali la kumi na tano la sheria ndogo

Ushuru wa huduma

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 4*

| <b>Na.</b> | <b>SAFU YA KWANZA</b>  | <b>SAFU YA PLI: kiasi cha ada</b>                         |
|------------|--|---|
| 1.         | Shughuli za kiuchumi na biashara zinazofanywa ndani ya eneo la Halmashauri kama vile kilimo, kandarasi, wafanyabishara, ufugaji, makampuni yaliyosajiliwa na yasiyosajiliwa [kif cha 7(1) z] | 0.3% ya mauzo ghafi baada ya kuondoa VAT na Exercise Duty |
| 2.         | Kushindwa kuleta taarifa za mauzo kama ilivyoelekezwa na Mkurugenzi  | Faini ya Tshs. 100,000/=                                  |
| 3.         | Kutoa taarifa za uongo   | 200,000/= kwa siku  |
| 4.         | Faini kwa makosa ya jumla  | 300,000/= kwa onyesho                                     |
| 5.         | Mkurugenzi kuhawilisha kosa pale mtu akikiri kwa maandishi   | Kiwango cha ushuru anachodaiwa                            |

Jedwali la kumi na sita la sheria ndogo

Ushuru wa mazao ya kilimo na mazao bahari

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 4*

| <b>Na.</b> | <b>SAFU YA KWANZA</b>  | <b>SAFU YA PLI: kiasi cha ada</b>                  |
|------------|--|--|
| 1.         | Ushuru wa mazao ya kilimo kutoka kwa mnunuzi wa mazao [kif cha 7(1) g]   | 5% yabei ya kununulia mazao shambani               |
| 2.         | Mrahaba wa mapato ya maduhuli ya mazao ya misitu ya asili [leseni/mauzo] | 5% ya kiwango kilicholipwa                         |
| 3.         | Ushuru wa samaki mnadani   | 5% ya bei ya kununua samaki mnadani                |
| 4.         | Leseni ya uvuvi  | Kulingana na viwango vilivyotolewa na Serikali Kuu |
| 5.         | Leseni ya usajili wa vyombo vya kuvulia samaki                           | Kulingana na viwango vilivyotolewa na Serikali Kuu |
| 6.         | Kutorosha mazao bila kulipa ushuru                                       | Faini ya Tshs. 300,000/=                           |
| 7.         | Kutoa taarifa za uongo   | 200,000/= kwa siku                                 |
| 8.         | Faini kwa makosa ya jumla  | 300,000/= kwa onyesho                              |
| 9.         | Mkurugenzi kuhawilisha kosa pale mtu akikiri kwa maandishi               | Kiwango cha ushuru anachodaiwa                     |

---

Jedwali la kumi na saba la sheria ndogo

---

Vibali vya ujenzi

---

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 4*

| <b>Na.</b> | <b>SAFU YA KWANZA</b>   | <b>SAFU YA PLI: kiasi cha ada</b> |
|------------|---|-----------------------------------|
| 1.         | Kwa jengo la ghorofa  | 100,000/=                         |
| 2.         | Taasisi/viwanda   | 50,000/=                          |
| 3.         | Biashara  | 50,000/=                          |
| 4.         | Makazi  | 50,000/=                          |
| 5.         | Minara ya simu  | 20,000/=                          |
| 6.         | Kwa jengo la ghorofa  | 100,000/=                         |
| 7.         | Ukaguzi wa ramani   | 20,000/=                          |
| 8.         | Faini kwa makosa ya jumla   | 300,000/= kwa onyesho             |
| 9.         | Mkurugenzi kuhawilisha kosa pale mtu akikiri kwa maandishi  | Kiwango cha ushuru anachodaiwa    |
| 10.        | Mkurugenzi anaweza kukagua majengo na kulipisha ambazo hazikukaguliwa na kupewa kibali cha ujenzi | Faini 50,000/=                    |

---

Jedwali la kumi na nane la sheria ndogo

---

Usajili wa vikundi vya kijamii

---

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 4*

| <b>Na.</b> | <b>SAFU YA KWANZA</b>                                | <b>SAFU YA PLI: kiasi cha ada</b> |
|------------|--|-----------------------------------|
| 1.         | Wanaosajiliwa chini ya maendeleo ya jamii            | 20,000/=                          |
| 2.         | Wanaosajiliwa chini ya idara nyingine za halmashauri | 30,000/=                          |

Jedwali la kumi na tisa la sheria ndogo: "A"

Ukusanyaji wa taka ngumu

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 4*

| Na. | SAFU YA KWANZA               | SAFU YA PLI: kiasi cha adakwa mwezi |
|-----|------------------------------|-------------------------------------|
| 1.  | Duka la jumla                | 3,000/=                             |
| 2.  | Duka la rejareja             | 2,000/=                             |
| 3.  | Nyumba ya makazi             | 2,000/=                             |
| 4.  | Viwanda                      | 25,000/=                            |
| 5.  | Mahoteli Makubwa             | 15,000/=                            |
| 6.  | Hoteli ndogo [mgahawa]       | 10,000/=                            |
| 7.  | Hospitali                    | 20,000/=                            |
| 8.  | ituo vya Afya/Zahanati       | 10,000/=                            |
| 9.  | Ofisi                        | 2,000/=                             |
| 10. | Wakandarasi                  | 15,000/=                            |
| 11. | Maduka ya vipuli             | 3,000/=                             |
| 12. | Ofisi za mawakili            | 2,000/=                             |
| 13. | Ofisi za uchaoaji na Shajala | 3,000/=                             |
| 14. | Nyumba za Wageni             | 5,000/=                             |
| 15. | Restaurants/Food kiosk       | 3,000/=                             |
| 16. | Garden refuse                | 35,000/= kwa tripu                  |
| 17. | Biashara nyingine yoyote     | 2,000/=                             |
| 18. | Vizimba                      | 100/= @ siku                        |

Jedwali la kumi na tisa la sheria ndogo: "B"

GHARAMA YA KADI ZA AFYA

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 4*

| Na. | SAFU YA KWANZA: aina ya biashara | SAFU YA PLI: kiasi cha adakwa mwezi |
|-----|----------------------------------|-------------------------------------|
| 1.  | Duka la rejareja                 | 5, 000/=                            |
| 2.  | Duka la jumla                    | 10,000/=                            |
| 3.  | Viwanda                          | 25,000/=                            |
| 4.  | Hoteli kubwa                     | 15,000/=                            |
| 5.  | Hoteli ndogo                     | 10,000/=                            |
| 6.  | Hospitali                        | 20,000/=                            |
| 7.  | Kituo cha Afya/Zahanati          | 10,000/=                            |
| 8.  | Ofisi                            | 5, 000/=                            |
| 9.  | Wakandarasi                      | 15,000/=                            |
| 10. | Maduka ya vipuli                 | 10,000/=                            |
| 11. | Ofisi ya wakili                  | 5,000/=                             |

|     |                              |          |
|-----|------------------------------|----------|
| 12. | Ofisi ya uchaoaji na shajala | 10,000/= |
| 13. | Nyumba za wageni             | 10,000/= |
| 14. | Mgahawa                      | 5,000/=  |
| 15. | Gereji                       | 15,000/= |
| 16. | Ghala                        | 10,000/= |
| 17. | Pharmacy/Maduka ya dawa      | 10,000/= |
| 18. | Vituo vya mafuta (sheli)     | 10,000/= |
| 19. | Mashine za kusaga            | 10,000/= |
| 20. | Workshops                    | 10,000/= |
| 21. | Biashara nyingine yoyote     | 5,000/=  |

\_\_\_\_\_

Jedwali la kumi na tisa la sheria ndogo: "C"

\_\_\_\_\_

**ADA YA UKAGUZI**

\_\_\_\_\_

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 4*

- (a) Ada Tshs 10,000/= italipwa kwa leseni mpya na Tshs 5,000/= kwa leseni za zamani, malipo haya yatalipwa kwa Halmashauri (afisa afya) kabla ya kutolewa kwa leseni mpya au kwa leseni ya zamani.
- (b) Ada ya Tshs 2,500/= italipwa kila pale Afisa Afya atakapofanya ukaguzi.

\_\_\_\_\_

Jedwali la kumi na tisa la sheria ndogo: "D"

\_\_\_\_\_

**ADA ZA UZOAJI MAJI MACHAFU**  
[Cesspit Emptying Charges]

\_\_\_\_\_

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 4*

\_\_\_\_\_

Ada ya uzoaji maji machafu [Cesspit emptying charges] ya shilingi 45,000/= kwa ajili ya biashara, viwanda au majengo ya taasisi, na 35,000/= kwa ajili ya nyumba za makazi malipo haya yatafanyika kabla ya kutoa huduma kwa Halmashauri au wakala wake.

\_\_\_\_\_

Jedwali la kumi na tisa la sheria ndogo: "E"

---

ADA YA FOMU YA VIPIMO VYA AFYA

---

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 4*

---

Kila mtu anayefanya kazi kwenye maeneo yanayoshughulika na vyakula au mazingira hatarishi atalazimika kulipa shilingi 2,000/= kwa Halmashauri kwa ajili ya vipimo kabla ya hajapatiwa hati inayothibitisha afya yake.

---

Jedwali la kumi na tisa la sheria ndogo: "E"

---

FOMU YA VIPIMO VYA AFYA

---

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 4*

---

Mimi..... Nakiri mbele ya Afisa Mtendaji wa Mji wa Muheza kwamba mnamo tarehe ..... Mwezi ..... Mwaka ..... nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya kulipa Ada za Usafi wa Mazingira na Ukaguzi wa Majengo ya Biashara. Nipo tayari kulipa kiasi cha ada ninachodaiwa pamoja na faini ya shilingi ..... ikiwa Afisa Mtendaji wa Mji/Mkurugenzi Mtendaji aliyopewa chini ya Sheria Ndogo hizi. Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni ya kweli nimeyatoa kwa hiyari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ilibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuata azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 31 mwezi wa 10 Mwaka 2012 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya:

Ibrahim Matovu  
MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYA  
MUHEZA

Amir Abdulrahman Kiroboto  
MWENYEKITI WA HALMASHAURI YA WILAYA  
MUHEZA

Nakubali

Mhe. MIZENGO P. PINDA (Mb)  
WAZIRI MKUU

DODOMA.

Tarehe.....